TANGAZO LA SERIKALI NA. 696 la tarehe 02 /12/2022

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA MTISI YA MWAKA, 2022

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Mtisi ya Mwaka, 2022.

Kutangazwa kwa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango wa jumla na kina wa eneo

3. Mpango wa jumla na wa kina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo.

**JEDWALI**

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la Upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P1 yenye majira - nukta 293689.051E, 9278973.719N karibu na Mto Mtisi; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Magharibi katika uelekeo wa N 04º 53' 03" E hadi alama ya mpaka ya upimaji namba P2 yenye majira - nukta 294029.948E, 9282963.097N; kwa umbali wa kilomita 4.003, baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Mashariki katika uelekeo wa N 09º 55' 40" E hadi alama ya mpaka ya upimaji namba WL 646 yenye maira - nukta 294471.000E, 9285483.000N; kwa umbali wa kilomita 2.558, baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Magharibi kwa uelekeo wa N 84º 26' 55" W hadi alama ya mpaka ya upimaji namba WL 650 yenye majira - nukta 292619.000E, 9285663.000N kwa umbali wa kilomita 1.860; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Magharibi katika uelekeo wa N 68º 13' 54" W hadi alama ya upimaji namba WL 649 yenye majira - nukta 291124.000E, 9286260.000N kwa umbali wa kilomita 1.609; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa S 20º 10' 35" W hadi alama ya mpaka ya upimaji namba WL 648 yenye majira - nukta 290119.000E, 9283525.000N kwa

umbali wa kilomita 2.913; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Mashariki kwa uelekeo wa S $34^{o}$ 58’ 55” E kwa kufuata mto Mtisi hadi alama ya mpaka ya upimaji namba WL 647 yenye majira - nukta 290387.000E, 9283142.000N kwa umbali wa kilomita 0.467; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi katika uelekeo wa S $29^{o}$ 47’ 26” W hadi alama ya mpaka namba WL 705 yenye majira ya nukta 289226.000E, 9281114.000N kwa umbali wa kilomita 2.336; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Mashariki katika uelekeo wa S $19^{o}$ 58’ 21” W hadi alama ya mpaka ya upimaji namba WL 692 yenye majira - nukta 290337.000E, 9278057.000N kwa umbali wa kilomita 3.253; baada ya hapo mpaka unaeleka Kaskazini – Mashariki kwa uelekeo wa N $18^{o}$ 22’ 05” E hadi alama ya mpaka ya upimaji namba WL 663 yenye majira - nukta 290763.000E, 9279340.000N kwa umbali wa kilomita 1.351 karibu na mto Magula; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Mashariki katika ueleko wa S $82^{o}$ 51’ 55” E hadi ulipoanzia”.

Dodoma,
8 Novemba, 2022

ANGELINE S. MABULA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*